MAMBO YAMPASAYO MWISLAMU KUYAJUA NA KUYAAMINI

Kimeandikwa na
Hujjatul Islam S.S. Akhtar Rizvi

Kimetafsiriwa na
Maalim Dhikiri U.M. Kiondo

Kimetolewa na
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033,
DAR ES SALAAM, TANZANIA.

MAMBO YAMPASAYO MUISLAMU KUYAJUA NA KUYAAMINI

Kimeandikwa na:

Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi

Kimetafsiriwa na:

Maalim Dhikiri U. M. Kiondo

Kimetolewa na Kimechapishwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033
Dar es Salaam - Tanzania

Haki za kunakili imehifadhiwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania

ISBN 9976 956 57 6

Toleo la Kwanza	1990:	Nakala 2500
Toleo la Pili	1993:	Nakala 1000
Toleo la Tatu	1995:	Nakala 1000
Toleo la Nne	1997:	Nakala 1000
Toleo la Tano	1999:	Nakala 1000
Toleo la Sita	2001:	Nakala 1000
Toleo la Saba	2004:	Nakala 1000

Kimetolewa na Kimechapishwa na::
BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA
S.L.P 20033
DAR ES SALAAM - TANZANIA

YALIYOMO

Shukrani 1
Dibaji 2
Majukumu Saba 6
Usul-e-deen 10
Madhambi Makubwa 15
Maelezo ya baadhi ya Istilahi za Kiislamu 19
Zaruriyat-e-deen 25
Aina kumi na Nne za Watu 29

SHUKRANI

Kitabu hiki ni tafsiri ya kitabu cha Kiingereza kiitwacho "*What a Muslim should know and believe*" kilichoandikwa na Hujjatul Islam, Maulana Sayyid Saeed Akhtar Rizvi.

Baada ya kukiona kuwa ni kitabu kifaacho kuwazindua wazazi wa Kiislamu juu ya Uislamu wao na wa vijana wao na hasa waahidiwa tumeona tukitafsiri kwa lugha ya Kiswahili.

Tunaomba Allah (s.w.t.) atujaalie usikivu wa kutuwezesha kunufaika kutokana na juhudi za ndugu yetu Maulana Sayyid Saeed Akhtar Rizvi – Aamina.

Mfasiri

DIBAJI

Mwanachuoni maarufu, Marehemu Shaykh Ja'far Shushtari[1] aliandika kijitabu kidogo kiitwacho *Manhaju 'r-rishad*, kizungumziacho juu ya mambo yaliyo misingi ya Dini, yenye kumpasa kila Mwislamu kuijua. Baadaye, mtu fulani alikiunga kijitabu hiki na vijitabu vingine kadhaa vya *Fiqih* na mkusanyo huo akauita *Majma'u 'r-risa'il* ambao ulitumika kuwa '*amaliyyah*[2] kwa muda mrefu.

Baada ya kufariki kwa Marehemu Sayyid Abul-Hassan Isfihani (mnamo mwaka 1365 Hijiriya / 1946 Masihiya). Mashia wa Bara Hindi (kama walivyofanya ndugu zao wa nchi nyinginezo), walifanya *Taqleed* ya Marehemu Sayyid Hussayn Brojardi (wa Qum, Iran), baadhi ya '*Ulama* walizitafsiri '*amaliyyah* za Marehemu Sayyid Hussayn Brojardi kwa lugha ya Kiurdu. Miongoni mwa '*Ulama* waliofanya hivyo ni Sayyid Qamaru 'z-Zaman, aliyekitafsiri kile kitabu *Majma'u 'r-risa'il* na akatia maelezo cha Sayyid Brojardi chini ya kurasa, akakiita kitabu hicho, *Jami'u 'l-masa'il*.[3]

Mnamo mwaka 1950 Marehemu Sayyid Khadim Husayn (wa Faizabad, India)[4] alikitafsiri kile kitabu kiitwacho *Manhaju 'r-rishad* tu kutoka kwenye kile kitabu kiitwacho *Majma'u 'r-risa'il* na akakiita *Tuhfatu 'l-'ibad*.[5]

Nilipokuwa nikikiandika kitabu *Day of Judgement* mnamo mwaka 1974 nilitaka nikitie humo baadhi ya mambo yaliyoelezwa na Marehemu Shaykh Ja'far Shushtari kwa sababu, kwa ujumla mambo hayo hayapatikani

1 Sheikh Ja'far Shushtari alifariki mnamo mwaka 1303 Hijiriya. Yeye yu mwandishi wa kile kitabu maarufu kiitwacho *Al-Khasa'isu 'l-Husayniyyah*.

2 Kitabu hiki kilikuwa na maamrisho ya *Fiqih* (Sheria za Dini) au *shari'ah* na kilitayarishwa kitumiwe na *Muqallidin* (wafuasi) wa *Mujtahid* (Mwana chuoni wa kidini mwenye madaraka ya kutoa hukumu (*Fatwah*) juu ya masuala ya kidini). Kitendo cha kumfuata *Mujtahid* katika hukumu za *shari'ah* ya Dini kinaitwa *Taqleed*.

3 Kitabu hiki kilitolewa na "Kutub Khana Husayniyyah", Lahore, (Pakistan).

4 Marehemu Sayyid Khadim alifariki mjini Mombasa (Kenya) mnamo mwaka 1969.

5 Kitabu hiki kilichapishwa kikiwa ni "Nyongeza" ya gazeti (la kila mwezi) liitwalo *al-Jawad* la mjini Varanasi (India), toleo la Juni-Julai 1950.

kwenye '*amaliyyah* nyinginezo, lakini kwa bahati mbaya sikupata kitabu chochote kati ya viatabu hivyo pale mjini Dar es Salaam.

Nilitoka Afrika ya Mashariki kwenye mwezi wa Agosti mwaka 1978. Lakini kwa mapenzi ya Allah nimerudi tena mwaka huu, mnamo mwezi wa Februari, kwa ajili ya ziyara fupi tu.

Mnamo mwezi Mei, nilipokuwa mjini Mombasa, niliipata nakala ya *Jami'u 'l-masa'il* kwenye maktaba ya rafiki yangu wa tangu zamani sana na mwenyeji wangu, Haji Ali Mohammad Jaffer Shariff.[6] Nilimwonyesha sehemu hiyo niliyoitaja hapo juu ambamo mwandishi aliyataja mambo sita yaliyo muhimu kwa mtoto kuyajua au kuyatekeleza afikiapo *baligh* (balehe). Vile vile nilimwonyesha maelezo juu ya aina mbali mbali za watu kwa mujibu wa itikadi na matendo yao. Haji Ali aliniomba nizitafsiri sehemu hizo mbili kwa lugha ya Kiingereza ili watu wetu waweze kuyajua na kufaidika kutokana na ujuzi huo.

Mnamo mwaka 1974 nilikwenda Iran kwa safari ya muda wa juma moja hivi. Haukuwepo muda wa kutosha; hivyo niliamua kwenda Mash-had asubuhi na kurudi mjini Tehran jioni yake. Ndugu Dhikiri Omari Kiondo (ambaye siku hizi yu Mhariri wa *Sauti ya Bilal*) alikuweko mjini Tehran akijifunza mafunzo ya juu ya Kiislamu chini ya uangalizi wa "World Organization for Islamic Services." Kwa maombi ya Viongozi wa taasisi hiyo, Ndugu Dhikiri alifuatana nami kwenye *Ziyarat* hiyo. Tulipokuwa kwenye Uwanja wa ndege wa Mash-had, nilimshauri Ndugu Dhikiri kwamba ingelikuwa vizuri tumtembelee kwanza Ayatullah Milani ili tukamtolee heshima zetu na baada ya hapo tutaweza kubakia kwenye Kuba Takatifu (la Imamu Ali ar-Ridha (a.s.)) tukifanya ibada zetu, pasi na kuliwazia jambo lolote jingine hadi muda wetu tuwezao kukaa mjini humo utakapomalizika. Baada ya hapo tuende uwanjani moja kwa moja kutoka hapo.

6 Haji Ali Mohammad Jaffer Sheriff yu mmoja wa Waasisi (waanzilishi) wa Bilal Musim Mission; hadi katika umri wake huu mkuu bado anautumia muda wake wote katika kazi hii tukufu ya *tabligh* (kuihubiri Dini).

Mara tu baada ya kuwasili nyumbani kwa Ayatullah Milani, mjukuu wake, Hujjatul Islam Fazil Milani alinileta Ndugu mmoja Mmarikani aliyetaka kuingia Uislamu wa kweli na akaniomba nimfundishe kijana huyo wa Kimarikani mambo muhimu ya Ushia ili kwamba atakapoitamka *Kalimah* aweze kuyajua mambo yaliyomo kwenye Ushia na wajibu anazojichukulia.

Kwa kushikiliwa zaidi na ingawa sikuwa na muda, niliitumia zaidi ya saa moja na nusu nikiwa pamoja na kijana huyo, naye akawa Shia. Nikijua muda wangu ni mfupi mno, nililazimika kuchagua kumfundisha yale mambo yaliyo muhimu zaidi katika huo muda mfupi na tukio hilo lilinipa tena mzingatio wa yale mambo sita muhimu aliyoyataja Marehemu Shaykh Ja'far Shushtari.

Tokea mwaka huo, Ndugu wengi waliokuwa wakijishughulisha na kazi ya *tabligh* wamekuwa wakiomba kijitabu chenye orodha ya mambo wapasikayo kumfundisha mhidiwa mpya aamuapo kusilimu.

Ninategemea kwamba sura tatu za mwanzoni mwa kijitabu hiki zitafaa kuwa mwongozo kwa wale wazazi wenye watoto wanaofikia balehe pamoja na wale wahubiri wanaowaingiza watu kwenye Uislamu wa kweli. Kwa ufupi kitawaonyesha kwamba ni lazima wafuasi wao wayaamini na wayatekeleze kimatendo mambo hayo mara tu wafikiapo balehe au wanaposilimu.

Kijitabu hiki si tafsiri ya neno kwa neno. Maelezo mengi yameachwa na mpango wa maudhui umebadilishwa tena. Vile vile imeonekana umuhimu wa kuzifafanua fikara nyingi na kuongezea maelezo mengi hapa na pale ili kuzifanya maudhui hizo zieleweke kiakili kwa msomaji wa Kiswahili asiye na ujuzi wa kutosha wa Elimu ya Theolojia ya Kiislamu wala wa istilahi zake. Orodha ya dhambi kubwa na ya baadhi ya *Zaruriyat-e-deen* na *Zaruriyat-e-madh-hab* zimechukuliwa kutoka kwenye vitabu vinginevyo.

Kama tulivyoeleza hapo juu Marehemu Ayatullah Brojardi aliandika maelezo ya chini ya kurasa kwenye hicho kitabu cha asili. Nilipokuwa nikitafsiri, nimeyafuata hayo maelezo yake; na ulipotokea umuhimu,

nimeyabadili kulingana na hukumu (*fatwah*) ya Ayatullah Sayyid Abul-Qasim al-Khoui.

Toleo la Kiingereza la kitabu hiki lilianzwa kuandikwa huko Mombasa (Kenya) mnamo tarehe 22 Shaaban mwaka 1405 Hijiriya (13 Mei 1985), lakini kwa sababu hii au ile hakikuweza kumalizika hadi leo, ambapo niko hapa Nakuru (Kenya) kwa kipindi cha mwezi mmoja hivi. Kwa bahati nzuri, mwenyeji wangu hapa, Haji Husain A. M. Jaffer amebahatika kuwa na nakala ya kitabu *Tuhfatu 'l-'ibad* tulichokitaja hapo juu na nimeyalinganisha maandishi haya na kijitabu hicho pia.

وَمَا تَوْفِيقِي إِلاَّ بِاللهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ

WAMAA TAWFIQI-ILLAA BILLAHI-ALAYH
TAWAKKALTU WAILAYHI UNIYBU.

(Na hakuna yeyote mwenye Taufiki ila kutoka kwa Allah (tu) na Kwake ninalejea).

Kwa sasa
niko Nakuru (Kenya)
2 Shawwal 1405
20 Juni, 1985

Sayyid Saeed Akhtar Rizvi
Mkurugenzi Mkuu
World Ahlul Bayt (a.s.)
Islamic League,
London

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

الحمد لله رب العلمين و الصلو ة و السلام على
خير خلقه محمد و اله لطاهرين

SURA YA 1
MAJUKUMU SABA (7)

Sisi wanadamu si wenye kuishi milele; tunao mwanzo na mwisho. Vile vile si wenye kujifanya kuweko wenyewe. Ni lazima kwamba alikuweko Muumba aliyetuumba na kutufanya tuwepo. Muumba huyo ni Allah, aliye huru kutokana na upungufu wowote na makosa.

Kuifanya kazi bila ya sababu au shabaha ni upungufu. Hatupendi mtu yoyote yule atulaumu kwa kufanya kazi bila ya shabaha. Hali kadhalika Allah naye, ni lazima kwamba katuumba kwa sababu/shabaha iliyo nzuri. Allah analizungumzia jambo hili anapowauliza wanadamu kwenye Qur'ani tukufu akisema: "*Je mlidhani ya kwamba Tumekuumbeni bure na ya kwamba hamtarudishwa Kwetu?*" (Qur'ani 23:115). Hivyo iko shabaha ya kuumbwa kwetu.

Tumekajua ulimwenguni hapa, tunaishi maisha yaliyo jaa wasi wasi na msukumo na kisha tunakufa. Je, hii ndiyo shabaha ya maisha yetu? Hapana! Matatizo haya yanatokana na maisha, wala si shabaha ya maisha yetu. Ni lazima kwamba hiyo shabaha iwe ni tofauti kabisa na hayo maisha yenyewe.

Je, utajiri, afya njema na madaraka ndizo shabaha za maisha yetu? Hapana! Vitu hivi ni njia tu za kuyachukulia maisha, wala siyo hiyo shabaha.

Je, kuitafuta heshima, umaarufu na madaraka ndizo shabaha za kuumbwa kwetu? Hapana! Hayo yote ni pande mbali mbali za maisha na wala sio shabaha yake. Ni lazima hiyo shabaha iwe jambo lililo kuu zaidi kuliko hayo maisha yenyewe.

Hebu tuuliza Muumba Mwenyewe kwa nini Ametuumba. Kama Anatuambia, ndiyo itakuwa sababu ya halisi na ya kweli. Na Yeye, katika huruma yake, tayari alituambia - bila ya sisi kuuliza. Yeye anasema: *Na sikuumba majinni na watu ila wapate kuniabud*u (Qur'ani 23:115).

Kila mwanaume na mwanamke ni lazima aitimize hii shabaha ya kuumbwa kwake. Ni lazima kila mmoja ajitoe ili kuyatimiza mapenzi ya Allah na amwabudu. Tunapomwabudu Allah tunaukubali utukufu na nguvu Zake na tunakiri kutokuwa kwetu na msaada na kuhitaji kwetu katika njia aliyoeleza yeye Allah, na tunafanya hivyo kwa nia ya uaminifu na moyo safi, kwa kumtii Allah ili tuweze kusogea karibu zaidi Naye.

Allah kawatuma Mitume (a.s.), akawateua Maimamu (a.s.), akavifunua vitabu, na akaziamrisha sheria za *shariʿah* ili kutuongozea kwenye njia iliyonyooka na kutufundisha njia sahihi ya kumuabudu Allah. Ni lazima tuufuate mwongozo wao kwa sababu ndiyo njia pekee itakayotuwezesha kulifikia lengo la maisha yetu na kuitimiza shabaha ya kuumbwa kwetu.

Allah kwa rehema Zake, hakuwaamrisha watoto au wendawazimu kulitimiza jukumu hili. Ni pale tu mtoto afikiapo balehe akiwa na akili timamu, ndipo atakapowajibika kuufuata mwongozo wa Allah tulioutaja hapo juu - yaani yale maamrisho ya *shariʿah*.

Mvulana hufikia utu uzima (huwa *baligh* بالغ au balehe) anapofikia umri wa miaka kumi na mitano au anapotoa manii (mbegu za uzazi awapo usingizini au yu macho) au nywele za mbeleni zianzapo kuota.

Msichana hufikia utu uzima anapofikia umri wa miaka tisa au aanzapo kuota nywele za mbeleni.

Mvulana au Msichana afikiapo utu uzima naye akiwa na akili timamu (yaani si mwenda wazimu au kichaa) anaitwa *mukallaf* مكلف (mke ni *mukallafah* مكلفة). Tunaweza kuitafsiri istilahi hii kwa maana ya yule mtu apasikaye kuyafuata maamrisho ya *shari'ah* au yule mtu achukuliwaye kuwa yu mwenye kupasika na maneno yake na vitendo vyake.

Mara tu baada ya mtu kuwa *mukallaf*, mtu hupasika na itikadi yake, maneno yake na matendo yake. Kabla ya hapo, kwa kawaida, mtu hawi muumini wala kafiri. Lakini mtoto wa Mwislamu anachukuliwa kuwa yu Mwislamu na mtoto wa asiyekuwa Mwislamu huchukuliwa kuwa yu asiyekuwa Mwislamu. Jambo hili linafuata msingi wa *taba'iyat* (تبعية yaani kufuata), ambao kwao, watoto hutawaliwa na zile hukumu ziwatawalazo wazazi wao.[1]

Ni wajibu juu ya kila mtu kuwa na itikadi iliyo sahihi afikiapo balehe. Hivyo basi, ili aweze kuyatekeleza kimatendo mambo yote yampasayo ni lazima ajitafutie elimu sahihi ya itikadi zilizo misingi ya Dini "Usul-e-deen" Mizizi ya Dini, kabla ya kufika huo muda wa "bulugh" بلوغ (= balehe, au utu uzima).

---

1 Maelezo ya hapo juu yanasimama kwenye msingi wa mtazamo wa ujumla. Lakini wakati mwingine hutokea kwamba wavulana wa miaka kumi wakapata fahamu na akili za kutosha kuweza kutofautisha baina ya ukweli na uwongo, kuweza kupambana baina ya lililo sahihi na lisilo sahihi, na wakachagua lililo sahihi na ukweli kuliko lile lisilo sahihi na lililo uwongo. Watoto wa aina hii ni Waislamu, na ukafiri wa wazazi wao hautachukuliwa dhidi yao. Hii ndiyo sababu iliyomfanya Shaykh Tusi (r.a.) aseme kwamba: "Jukumu la mtoto ni la aina mbili:-

   i. Jukumu la kuitafuta itikadi ya kweli na dini iliyo sahihi. Jukumu hili huanzia kwa mvulana afikiapo umri wa miaka kumi.
   ii. Jukumu la kuyafuata na kuyatekeleza maamrisho ya *shari'ah*. Jukumu hili huanzia kwa mvulana afikiapo umri wa miaka kumi na mitano."

   Hivyo ndivyo isemavyo *Fatwah* ya Sayyid Kazim Yazdi katika kitabu chake *al-Urwatu 'l-wuthqa* ambacho Mujtahid wote wengine huikubali. Sayyid Mohsin al-Hakim ameendelea zaidi. Kkwa mujibu wake, japo Uislamu wa mtoto huyo usisimame kwenye msingi wa kuelewa kihoja (yaani awe kavutiwa na watu fulani au jamii anayoishi nayo) itakubalika na atakuwa ya Mwislamu.

Yako mambo SABA yampasayo *mukallaf* kuyazingatia anapofikia balehe. Mambo hayo ni haya:-

1. Mizizi ya Dini, *Usul-e-deen*.
2. Kujifunza *salat* (kwa vitendo kama bado hajajifunza).
3. Kama wakati wa utotoni kafanya jambo lolote limwajibishalo kufanya *ghusl* (kwa mfano kuigusa maiti) basi itampasa afanye *ghusl* mara moja ili *salat* zake na amali hizo zisihi.
4. Ajifunze hukumu za *salat* zilizo muhimu na mambo mengine ya wajibu kama vile funga, n.k. (kama bado hajajifunza).
5. Kama anazo haki za watu wengine (kwa mfano madeni n.k.) ni lazima azilipe au awaombe wamsamehe.
6. Ni lazima ajifunze hukumu za *shari'ah* zilizo muhimu kuhusiana na kazi yake (kama vile biashara, ushirikiano katika biashara, uajiri, kukodi n.k.) ili mapato yake yawe halali.
7. Ni lazima azijue dhambi kubwa, ili aweze kujiepusha nazo. Vile vile ni lazima avijue vitu vingine vilivyo haramu ili aweze kuviambaa.[2]

Hukumu hii yampasa mwenye kusilimu kuizingatia baada ya kuutumia muda wake fulani katika *kufr* (kufuru).

Ili kuyapata maelezo ya kimantiki ya Mizizi ya Dini msomaji wetu anaombwa akisome kitabu changu *Uislamu*.[3] Lakini maelezo mafupi ya mambo yake muhimu tutayatoa kitabuni humu. Maelezo hayo yatafuatiwa na orodha ya dhambi kubwa.

2 Kitabu cha asili kimetaja majukumu sita tu, kimeunga "Elimu ya vitu haramu" na lile jukumu la sita. Mimi nimeiorodhesha elimu hiyo peke yake, kwa sababu ya umuhimu wake ulio mkuu.

3 Taasisi ya World Organization for Islamic Services (WOFIS) ya mjini Tehran (Iran) imekitafsiri kitabu hiki *Islam* katika lugha za Kitaliani, Kijapani, Kithai, Kiindonesia, na Kihausa, na tafsiri yake ya Kiswahili imetolewa na Bilal Muslim Mission of Tanzania ya mjini Dar es Salaam.

SURA YA 2

USUL-E-DEEN

Itikadi kubwa zinaitwa *Usul-e-deen* yaani Mizizi ya Dini, *Usul-e-deen* ni tano.

Tatu kati yao zinaitwa *Usul-e-Islam* – Yaani Mizizi ya Uislamu. Hizi ni:-

1. *Tawhid* – Kuamini Upweke wa Allah.
2. *Nubuwwat* – Kuiamini Mitume.
3. *Qiyamat* – Kuiamini Siku ya Hukumu.

Usul-e-deen mbili zilizosalia zinaitwa *Usul-e-Iman* – yaani Mizizi ya Imani. Hizo nazo ni:-

4. *Adl* - Kuamini Uadilifu wa Allah.
5. *Imamat* - Kuamini Kuirithi nafasi ya Mtume (s.a.w.w.).

Mtu anayeziamini hizi *Usul-e-deen* tano anaitwa *Shi'a Ithna 'ashariyah*. *Shi'a* huyo huamini kwamba: -

1. **Tawhid:** Kuna Mungu mmoja tu aitwaye (Allah), aliye wa tangu na tangu na wa milele, Ajitoshelezaye, Hana mwanzo wala mwisho, Mwenyezi, Yu Mwenye uwezo juu ya kila kitu na kila jambo; Yu Mjuzi wa yote, Anaijua kila kitu, hakuna lolote lililo siri Kwake. Ana hiari katika kila jambo, Hana anachokifanya kwa kulazimishwa. Yu Mwenye kutambua kila kitu, Yu Mwenye kusikia kila kitu, Yu Mwenye kuona kila kitu, Mwenye kuwepo kila mahali. Anaona na kusikia kila wazo la mtu (ingawa hana macho wala masikio), Hana mshirika wala Mwenzi, Hana Mwana, binti wala mke. Hakutengenezwa wala Hakuundwa kwa kitu chochote cha kimaada. Hana mwili wala hayuko mahali fulani

maalumu. Haathiriwi na chochote chenye kuhusiana na umbo la mwili. Hatawaliwi na muda, nafasi, badiliko au jambo lolote la aina hiyo. Haonekani, Hajawahi kuonekana, na katu Hataonekana iwe hapa duniani au kesho Akhera. Sifa zake hazikutengana na Nafsi Yake.

2. **Adl:** Allah Yu Mwadilifu; Hamwonei yeyote; Yeye katuamrisha tuwatendee uadilifu viumbe wenzetu – lakini Yeye Mwenyewe Anatutendea si uadilifu tu, bali na rehema pia. Ametuumba kwa ajili ya Ibada Yake, ili tuweze kuufikia ukamilifu wa kiroho kutokana na Ibada hiyo. Huo ukamilifu wa kiroho utatuwezesha kumkaribia Allah. Kwa ajili ya shabaha hiyo, katupa uhuru wa mapenzi na hiari ya kuchagua. Tunapoichagua Njia iliyonyooka (Aliyo tuamrisha Allah), Allah anatuthibitishia kwamba kesho Akhera tutapata furaha na utukufu, kwa Rehema Zake Allah.

3. **Nubuwwat:** Ili kutuonyesha Njia iliyonyooka, Allah Amekuwa akituletea sisi wanadamu wawakilishi wake. Wawakilishi hawa wanaitwa *Anbiya* (انبیاء -Manabii) na *Rusul* au *Mursaleen* (رُسُل au مرسلین = Marasuli). Neno *Anbiya* ni wingi. Umoja wake ni *Nabii* (نبی = Nabii) na maneno *Rusul* na *Mursaleen* ni wingi. Umoja wao ni *Rasul* (رسول = Rasuli).

Walikuja Manabii na Marasuli 124,000, wa kwanza wao akiwa ni Hadhrat Adam (a.s.) na wa mwisho wao ni Nabii Muhammad Mustafa (s.a.w.w.).

Manabii wote ni *Ma'sumeen* (معصومین = Wasio na dhambi na Watakatifu). Neno *Ma'sumeen* ni wingi. Umoja wake ni معصوم *Ma'sum* = Asiye na dhambi na Mtakatifu).

Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) yu Nabii wa Mwisho. Yeyote yule adaiye Utume baada yake yu mwongo na mzushi.

4. **Imamat:** Ili kuwaongoza watu kwenye njia iliyonyooka, na kuihifadhi dini ya Uislamu, Allah kawateua warithi 12 wa nafasi ya

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) walioishika nafasi hiyo mmoja baada ya mwingine. Warithi hawa huitwa *Aimmah* ائِمّة Maimamu au Viongozi). Neno *Aimmah* ni wingi. Umoja wake ni *Imam* إمام ambalo maana yake ya kawaida ni Kiongozi).

Wa kwanza wao alikuwa ni Hadhrat Ali bin Abi Talib (a.s.). Maimamu wote ni *Maʿsumeen*.

1. Ali bin Abi Talib al-Murtaza (a.s.)
2. Hasan bin Ali al-Mujtaba (a.s.)
3. Husain bin Ali Sayyidus-Shuhadaa (a.s.)
4. Ali bin Husain Zaynul Abideen (a.s.)
5. Muhammad bin Ali al-Baqir (a.s.)
6. Jaʿfar bin Muhammad as-Sadiq (a.s.)
7. Musa bin Jaʿfar al-Kadhim (a.s.)
8. Ali bin Musa ar-Ridha (a.s.)
9. Muhammad bin Ali at-Taqi (a.s.)
10. Ali bin Muhammad an-Naqi (a.s.)
11. Hasan bin Ali al-Askari (a.s.)
12. Muhammad bin Hasan al-Mahdi (a.s)

Imamu wa 12, Imamu Muhammad al-Mahdi (a.s.) bado yu hai lakini kafichwa machoni petu kwa amri ya Allah. Atadhihiri tena atakaporuhusiwa na Allah kuja kuudumisha Ufalme wa Allah hapa duniani. Itakuwa ni karibu na mwisho wa dunia, hapoatakapo udumiasha uadilifu na usawa hapa duniani baada ya hii dunia kujawa na dhulma na uonevu.

5. **Qiyamat:** Baada ya kutawala Imamu al-Mahdi (a.s.) kwa uadilifu na usawa ulimwenguni kote, kitafuatia *Qiyamat*, siku ya Ufufuo, siku ya Hukumu. Siku hiyo watu wote watakufa, kisha watu wote watafufuliwa ili waikabili Hesabu yao, itikadi yao na amali zao. Watu wenye itikadi sahihi na waliotenda amali njema watatiwa Peponi. Wale wenye itikadi isiyo sahihi watatiwa Motoni.

Kuzijua na kuzifuata *Usul-e-deen* tano tulizozitaja hapo juu ndilo jukumu la kwanza na lililo kuu zaidi kwa *Mukallaf*. Kama tulivyoeleza sasa hivi, kuziacha hizi *Usul-e-deen* humtupilia mtu kwenye adhabu ya milele ya Moto wa Jahannamu.

Kama mtu haziamini hizi *Usul-e-deen* basi Allah Hatazitakabalia amali zake za Ibada. Vile vile mtu huyu hastahili kupewa *Khums*, *Zakah*, *Fitrah*, *Radd-e-mazalim* na *Kaffara*.[4]

Kama tulivyoeleza hapo mwanzoni mtoto mdogo wa mzazi Mwuislamu huchukuliwa kuwa ni Muislamu. Lakini mara tu baada ya kuwa balehe ni lazima yeye mwenyewe awe na itikadi iliyo sahihi na imani iliyoshamiri vizuri. Kama katika muda huo atakuwa kazisahau hizi itikadi kuu, au ana shaka juu yao, italeta tatizo kubwa.

Kuzikiri kwa maneno tu hakutoshi. Ni lazima mtu huyo awe na itikadi madhubuti moyoni mwake.

Vile vile imesisitizwa sana katika Madhehebu ya *Shi'a Ithna 'ashari* kwamba ni lazima mtu huyu ajitafutie elimu ya *Usul-e-deen* kwa thibitisho na hoja. Kuhusiana na jambo hilo tunatofautiana kabisa na Wakristo. Wakristo wanasema, "Amini kwanza, kisha ndipo utaelewa." Sisi tunasema, "Kwanza Uelewe kisha ndipo uamini."

4 *Khums*, *Zakah*, *Fitrah*, *Radd-e-mazalim* ni aina mbalimbali za kodi za kidini zihusianazo na fedha.

Neno *Radd-e-mazalim* lina maana ya "Kuirudisha au kuiondoa mizigo au majukumu."

Kama Muislamu akiwa na pesa au mali ambayo kwa mujibu wa *shari'at* si yake, itakuwa wajibu juu ya Muislamu huyo kuzirudisha pesa hizi au mali hii kwa mwenyewe. Kama hawezi kumpata huyo mwenyewe au mrithi wake, basi pesa hizo au mali hiyo itaitwa *Mazlamah* ("Mizigo" au "Majukumu)"

Hivyo, ili Muislamu huyu aweze kujiondolea mzigo au jukumu hili atahitajika kuzitoa *Sadaqah* pesa hizo au mali hiyo kwa niaba ya huyo mwenyewe kumpa maskini Muislamu mwenye kustahili.

Hata hivyo, kama mtu hakujifunza thibitisho na hoja za kiakili, za *Usul-e-deen*, lakini anaziamini kwa nguvu, natuseme kwa sababu wazazi wake wamemwambia afanye hivyo, anakubaliwa kuwa *Shi'a Ithna 'ashari*. Lakini daima itikadi ya aina hiyo imo kwenye hali ya hatari. Mtu huyu anayaamini mambo haya kwa sababu anayo imani juu ya baba yake na mama yake. Vizuri sasa natufikirie kwamba kwenye maisha ya baadaye anakutana na mtu fulani ambaye anayo imani zaidi juu ya elimu yake na mtu huyo akamwambia kuwa hakuna Mungu au Imamu wa Kumi na mbili. Je, imani yake juu ya Mungu mmoja au Imamu wa kumi na mbili haitatikisika? Au hata kuvunjika kabisa? Hivyo basi, ni muhimu kwa wazazi kuwafundisha watoto wao mada muhimu ya *Usul-e-deen* kwa thibitisho za kiakili na kimantiki, ili kwamba isiwezekane kwa mtu yeyote kuwapoteza katika siku za baadaye.

SURA YA 3

MADHAMBI MAKUBWA

Allah Anasema kwenye Qur'ani Tukufu:
"Kama mkijiepusha na madhambi makubwa ambayo mnayokatazwa, Tutakufutieni madhambi yenu (madogo), na Tutakuingizeni (Peponi mahali pa) mwingizo mtukufu." (Qur'ani 4:31)

Hivyo basi, ni muhimu kwa *Mukallaf* kufahamu ni dhambi zipi zilizo kubwa ili aweze kuziambaa. Kwa njia hii, Allah kwa rehema zake, na kwa mujibu wa ahadi yake, atazighufiria dhambi zake ndogo zote na makosa yake.

Orodha ya madhambi makuu ifuatayo hapa chini imenukuliwa kutoka kitabu kiitwacho *Minhajus Saleheen* cha Ayatullah Sayyid Abul Qasim al-Khoui, Dama Zilluhu.

1. Kuitakidi kwamba Allah ana mwenzi wake au mshirika katika Uungu wake au kumwabudu yeyote yule asiyekuwa Allah.
2. Kukata tamaa juu ya rehema za Allah au kuitakidi kwamba Allah hatakuokoa katika siku ya Hukumu.
3. Kutomwogopa Allah, au kufikiria kwamba Allah hatakuadhibu kwa ajili ya dhambi zako.
4. Kuwatendea maovu wazazi wako; au kuwaasi; au kuzidharau fikara zao.
5. Kumuua mtu pasi na haki – yaani kumuua bila ya ruhusa ya kishariah.
6. Kumsingizia zinaa mwanamke aliyeolewa.
7. Kula pesa au mali ya yatima kwa njia isiyoruhusiwa na sharia na kwa dhulma.

8. Kukimbia kutoka kwenye *jihad* (Vita takatifu).
9. Kutumia au kula kitu fulani au pesa zilizotokana na riba.
10. Kutenda uzinzi au zinaa.
11. Kuangaliana kiashiki watu wa jinsia moja (kwa wanaume kufirana na wanawake kusagana).
12. (Kutumia) uchawi au uramali.
13. Kuapa kwa jina la Allah kwa jambo la uwongo.
14. Kuziacha *Salah* au jambo lolote lile la wajibu.
15. Kutotoa *zakah*.
16. Kutoa ushahidi wa uwongo.
17. Kuficha (yaani kutotoa) ushahidi wa kweli.
18. Kunywa ulevi au pombe.
19. Kuvunja ahadi.
20. Kuwatendea maovu ndugu wa damu au kutowatendea mema.
21. Kuihamia sehemu ambayo upo uwezekano wa kutokea hatari kwa upande wa dini au kwa upande wa wafuasi wa dini - yaani kuhamia mahali ambapo hutawezi kuzifuata *shari'ah* za dini pasi na vipingamizi.
22. Wizi au unyang'anyi.
23. Kuacha au kulikana jambo lolote lile ambalo Allah kamfunulia Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).
24. Kusema uwongo; na lililo ovu zaidi ni kusema uwongo dhidi au juu ya Allah, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Bibi Fatimah (a.s.) au Maimamu (a.s.).
25. Kula nyama n.k. ya mfu, au ya mnyama ambaye hakuchinjwa kwa mujibu wa *shari'ah*.
26. Kunywa au kula damu.
27. Kula nyama ya nguruwe, mafuta ya nguruwe au chochote kitokanacho na nguruwe.
28. Kucheza kamari.
29. Kutumia au kula kitu chochote kitokanacho na njia isiyo ya kihalali ya kujipatia maisha – kwa mfano kula kutokana na pesa zitokanazo na kuuza maiti, au pombe, au michezo ya kamari; pesa zilizotokana na hongo, au pesa zitokanazo na umalaya.
30. Kula rushwa ili utoe hukumu.

31. Kutowapa washtiri (wateja) vipimo kamili vya uzani au urefu au kuuza vitu kwa vipimo pungufu.
32. Kuficha vyakula – yaani kutoviuza wakati wa uhaba wao ili kusubiri bei ipande.
33. Kumsaidia mdhalimu na mtu asiyetenda haki, au kikundi cha watu wenye tabia hiyo; Kujiambatanisha nao au kuwatumikia.
34. Kutolipa *Wajib Huquq* (haki iliyo wajibu juu ya mtu isipokuwa pale mtu akosapo uwezo wa kulipia).
35. Kiburi (au majivuno).
36. Uhusuda (yaani "Hasad")
37. Isirafu (Kufuja mali).
38. Kuidharau ibada ya *Hajji*.
39. Kupigana dhidi ya marafiki wa Allah.
40. Muziki. Muziki ni sauti yenye kuendelezwa kwa aina aina za sauti zenye kuongezeka mara kwa mara, kama ifahamikavyo kwa watu wasio na hisia za kidini. (Hii ina maana kwamba, muziki ni ile sauti ikubaliwayo na watu wasio na hisia za kidini, kuwa ni muziki).
41. Kutumia ala za muziki, au kusikiliza muziki wa ala.
42. *Ghibat* (Kusengenya); Kumsengenya Muumini kwa maneno, ishara au matendo – Yaani kutaja au kudhihirisha upungufu wowote wa kimwili alionao hasa, fedheha ya kijamii, upungufu wa kidini au kiutu, au upungufu wowote ambao Muumini huyo hangetaka ufahamike kwa watu. Haina tofauti yoyote kama kutaja huko kutafanyika kwa maneno au kwa matendo au kwa ishara tu.
43. *Tuhmat* (Tuhuma): Kumtuhumu Muumini juu ya jambo asilohusika nalo au ambalo hakulitenda. Tuhuma ni dhambi kubwa zaidi kuliko *Ghibat*.
44. Kumtusi au kumkebehi au kumfedhehesha Muumin kwa njia yoyote ile.
45. Kujenga uadui na fujo miongoni mwa Waumini kwa uchonganifu.
46. Kufanya ukuwadi. Ukuwadi ni kutongozea watu wake na mabinti za watu ili wafanye nao uzinzi au zinaa.
47. Kughushi. Kughushi ni kuchanganya bidhaa za thamani duni na thamani kubwa, ili uziuze kwa bei kubwa.
48. Kutenda amali njema kwa nia ya kutaka uonwe na watu tu (badala ya kuitafuta radhi ya Allah tu).

49. Kuzirudia-rudia dhambi ndogo.
50. Kuichukulia dhambi kuwa ni jambo dogo tu, kwa sababu “dhambi mbaya zaidi ni ile ambayo mwenye kuitenda huichukulia kuwa ni jambo dogo tu.”

Orodha tuliyoitaja hapa ni dhambi kuu tu. Kama mtu akitaka kufahamu zaidi juu ya jambo hili tafadhali na asome vitabu vinginevyo vyenye kulizungimza jambo hili.

Nyingi ya dhambi tulizozitaja hapa juu ni majina yenye kupasika kutolewa adhabu katika sheria ya adhabu ya Kiislamu.

SURA YA 4

MAELEZO YA BAADHI YA ISTILAHI ZA KIISLAMU

Kwa bahati mbaya si watu wote waliomo kwenye Njia iliyonyooka. Kama ambavyo Allah karudia–rudia kusema kwenye Qur'ani Tukufu, idadi kubwa ya watu wameitoka dini ya kweli. Hivyo basi, Uislamu umewagawanya watu katika makundi mbali mbali tunayoyataja hapa chini:-

1. Muslim: - Mtu anayeamini na kuthibitisha kwamba yu Mungu mmoja tu, kwamba Muhammad (s.a.w.w.) yu Nabii na Rasuli wa mwisho, na kwamba itakuwepo siku ya mwisho, anaitwa "Muslim" (Muislamu). Vile vile tunaweza kusema kwamba mtu yoyoye anayeziamini *Usul-e-Islam* (Mizizi ya Uislamu tulizozitaja hapo mwanzo (yaani *Tawhid, Nubuwwat* na *Qiyamat*) yu "Muislamu".

2. *Shi'a*:- Muislamu ambaye vile vile anaamini kuwa Hadhrat Ali bin Abi Talib (a.s.) alikuwa Imamu wa Kwanza baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kuteuliwa na Allah anaitwa *Shi'a*.

3. *Shi'a Ithna 'ashari*:- Muislamu anayewaamini Maimamu 12 walioteuliwa na Allah (tuliowataja hapo mwanzoni) na yeyote anayeiamini *Adl* ya Allah anaitwa *Shi'a Ithna 'ashariyah*)
(Ithna 'asher اثناعشر = kumi na mbili; Ithna 'asheriyah اثنا عشرية = mwenye kuwaamini Maimamu kumi na wawili). Vile vile tunaweza kusema kwamba, yeyote yule anayeziamini *usul-e-deen* tano yu *Shi'a Ithna 'asheriyah.*

4. *Kafir*: Kama mtu hakuamini kuwepo kwa Allah au hauamini Upweke wa Allah, au hauamini Utume wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.), au hakuamini kuwepo kwa siku ya Hukumu, anaitwa *kafir* (كافر = Kafir). Wingi wa neno hili ni *Kuffar* (كفّار =Makafiri). Ili kuweza kuifafanua zaidi maana yaneno hili, tutawaita watu hawa, watu wasio Waislamu.

Watu wasio Waislamu wamegawanyika makundi makuu mawili:-

i. *Mushrik* (مشرک Mshirikina): Huyu ni mtu anayemwekea Mwenyezi Mungu mshirika mwenziwe, Wingi wa neno hili ni *Mushrikeen* (مشرکین=Washirikina).

ii. *Ahlul-kitab*: (أهل الكتاب Watu wa Kitabu). Hawa ni Wayahudi na Wakristo.

Viko vikundi vinavyodai kuwa ni Waislamu lakini kwa hakika wao ni *kuffar* na *shari'ah* ya *Shi'a Ithna 'ashari* ina wahesabu kuwa ni *kuffar*. Watu hao ni hawa:-

iii. Mtu aikanaye *Zaruriyat-e-deen*(ضروریات دین: Mtu yeyote aikanaye au aitkanaye au atiaye shaka juu ya yeyote kati ya *Zaruriyat-e-deen* (Mambo ambayo kila mmoja wetu huyakubali kuwa ni sehemu ya Uislamu). Kwa mfano: Pepo na Moto, Sala 5 za kila siku, na mambo mengi mengineyo. Mtu anayeyakana mambo hayo, au anayeyatilia shaka au anayetukana mambo hayo yu *kafir*, japo awe anaitamka *kalimah* mara mia kwa siku. (Tazama sura ya 5 ya kitabu hiki kwa maelezo zaidi).

iv. *Ghali*: (غالی = Aliyekithiri). Wingi wa neno hili ni *ghulat* (غُلَاة = Waliokithiri). Mtu yeyote mwenye kuamini kuwa yeyote kati ya Mitume au Maimamu alikuwa Mungu au kuwa Mungu kali-chukua umbo la Mtume au Imamu huyu, au kwamba yeyote kati ya Maimamu alikuwa Mtume ……. kwa kifupi ni kwamba, yeyote anayempa Mtume au Imamu cheo cha juu kuliko cheo chake cha kweli …… anaitwa *Ghali*. Mtu huyo ni *kafir* japo adai kuwa yu Muislamu.

v. *Khariji*: (خارجی = Aliyeitoka Dini). Wingi wa neno hili ni *khawarij* (خوارج Walioitoka Dini). Hawa ni watu waliojitenga na Hadhrat Ali bin Abi Talib (a.s.) baada ya mapatano baina yake na Muawiyyah, wakidai kwamba Hadhrat Ali (a.s.) amekuwa (Allah na atusamehe) *kafir*. *Khawarij* ni *kuffar* mbele ya *shari'ah*.

vi. *Nasibi* (ناصبی = Awachukiaye Maimamu 12). Wingi wa neno hili ni *Nawasib* نواصب (Wenye kuwachukia Maimamu). Mtu yeyote anayemchukia yeyote kati ya Maimamu 12 au anayemtukana ni *Nasibi*. *Nasibi* nae ni *kafir*.

vii. Mwenye kumtukana Mtume (s.a.w.w.) n.k.: Yeyote yule amtukanaye au atumiaye lugha mbaya juu ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), Bibi Fatimah (a.s.) au yeyote kati ya Maimamu 12, yu *kafir*.

Ziko hukumu fulani fulani zinazowatawala *kuffar* tuliowataja hapa juu. Hukumu hizo ni hizi:-

1. *Mushrik* ni Najis (نجس = Aliyenajisika au mchafu). Ama kuhusu wale watu wa Kitabu, (yaani Wayahudi na Wakristo) kuna maoni mbali mbali juu yao. Hivyo msomaji anaombwa asome '*amaliyyah* ya *mujtahid* wake.

2. Mwanaume Kafiri: Mwanaume asiye Muislamu haruhusiwi kumwoa mwanamke wa Kiislamu na mwanamke asiye Muislamu haruhusiwi kuolewa na mwanaume Muislamu. Tofauti iliyopo ni kwamba mwanamke wa Kikristo au Kiyahudi anaweza kuolewa na Muislamu kwa ndoa ya *Mut'ah* (ndoa ya muda maalum).

3. Kafir hamrithi Muislamu: Mtu asiye Muislamu hawezi kumrithi Muislamu japo udugu wao uwe karibu kiasi gani.

4. Kafir hamiliki Mtumwa Muislamu: Mtu asiye Muislamu hawezi kummiliki mtumwa Muislamu.

5. Mnyama aliyechinjwa na Kafiri ni mfu: Mnyama aliyechinjwa na mtu asiye Muislamu huchukuliwa kuwa ni mfu. Si halali kula nyama ya mnyama huyo.

6. Nyama, Shahamu na ngozi za kafiri: Nyama, shahamu na ngozi zimilikiwazo na mtu asiye Muislamu ni najisi mpaka mtu ajue kuwa kafiri huyo kavipata vitu hivyo kutoka kwa Muislamu.

7. Muislamu hawajibiki kumzika Kafiri: Si wajibu juu ya Muislamu kuendesha maziko ya mtu asiye Muislamu.

8. Kafiri Namba (vii) hapo juu: Kuna kanuni maalumu juu ya kundi la mwisho la Kafir, yaani yule anayemtukana au anayetumia lugha mbaya juu ya yeyote kati ya ma'sumeen 14; Ni *wajib* (wajibu au lazima) juu ya Muislamu yeyote awezaye, kumuua *kafir* huyu bila ya kuwepo haja yoyote ya kuipeleka kesi yake kwa *qadi* wa *shari'ah*.

Murtadd (مرتد =Mwenye kuritadi): Kuna aina maalumu ya *kafir* aitwaye *Murtadd* – yaani mtu asilimuye kisha akaukana Uislamu. Hali ya *Murtadd* ni mbaya zaidi kuliko ile ya ukafiri wake wa awali. Hapa chini tunazitaja baadhi ya hukumu zilizo muhimu juu ya *Murtadd*.

Murtadd wana aina mbili:- *Murtadd Fitri* na *Murtadd Milli*.

Murtadd Fitri: Huyu ni mtu ambaye wazazi wake wawili (au mmoja wao) walikuwa Waislamu wakati wa kutungwa mimba yake, na alipofikia utu uzima, akaukana Uislamu kwa hiari yake.

Hukumu zenye kumhusu *Murtadd Fitri* zinatofautiana kufuatana na jinsia (kuwa mume au mke) ya mkosefu huyo – yaani kuna hukumu tofauti kwa wanaume na wanawake.

i. Mwanaume aliye *Murtadd Fitri*: *Murtadd Fitri* mwanaume ni Najis. Mkewe huwa *haramu* kwake, lakini itambidi huyo mke kukaa *'Iddah*

ya kifo. Hata katika wakati wa uhai wake anaipoteza haki ya mali yake – baada ya kulipa madeni yake, na kitakachosalia hugawanyiwa warithi wake walio Waislamu. Na kutubia kwake hakutakubalika katika uhai wake, kwa mujibu wa hukumu maarufu za wanachuoni wetu. Lakini Ayatullah al-Khoui anasema kuwa kwa hakika kutubia kwake kunakubalika huko Akhera na vile vile kunakubalika hapa duniani kwa kiasi fulani. Hivyo basi, kama akitubia, atakuwa *tahir* (tohara), na kama mkewe wa zamani akikubali anaweza kumwoa tena kwa ndoa mpya.

Kwa ufupi ni kwamba, atachukuliwa kwamba ni Muislamu - lakini hata hivyo, hatapata madaraka juu ya mali yake ila tu pale warithi wake wahiaripo kumrudishia. Hivyo hivyo, hukumu ya kifo haitaondolewa juu yake hata baada ya kutubia.

ii. Mwanamke *Murtadd Fitri*: kama mwanamke akiwa *Murtadd* (*Fitri*), huwa *najis* na huwa *haramu* kwa mumewe, lakini haipotezi mali yake, hahukumiwi kifo, na kutubia kwake kunakubalika. Kama akikataa kutubia, atafungwa.

Murtadd Milli: Huyu ni mtu aliyezaliwa na wazazi wasio Waislamu, na yeye mwenyewe alipofikia utu uzima akasilimu, na baadaye akaukana Uislamu.

Kafir huyu ni lazima aambiwe atubie, kama akitubia katika kipindi cha muda wa siku tatu tangu kuritadi kwake kutakubalika. Kama atakataa kutubia, atauawa kwenye siku ya nne. Mkewe aliye Muislamu atakuwa *haramu* kwake, yaani ndoa yao itabatilika pale pale, na huyo mwanamke itambidi akae *'Iddah* ya talaka kama walifanya ngono baada ya kuozwa; lakini kama kafiri huyo akatubia wakati wa *'Iddah* ya mkewe, ndoa yao itasihi pasi na haja ya kufanyika *Nikah* mpya.

Murtadd Milli anazuiwa kuitawala mali yake, (ingawa anabakia kuwa mwenye kuimiliki). Kama akitubia, atapata utawala, akikataa kutubia, atapewa mahitaji yake ya maisha hadi afe; na baada ya kufa kwake mali yake itagaiwa warithi wake walio Waislamu.

(Kwa maelezo zaidi ju ya jambo hili msomaji anaombwa asome vitabu vya *Fiqih* vyenye maelezo zaidi juu ya hukumu za makafiri hawa - *Murtadd Fitri* na *Murtadd Milli*).

Sasa tunaijia aina ya mtu ambaye Qur'ani inamwita *Munafiq* (منافق). Wingi wa neno hili ni *Munafiqun* (منافقون = Wanafiki). *Munafiq* ni mtu adaiye kuwa kasilimu, lakini kwa kweli hauamini Uislamu.

Mtu huyu huchukuliwa kuwa ni Muislamu maishani mwake. Mwili wake ni *tahir* (tohara), anaweza kuoa au kuolewa na Muislamu. Anaweza kumrithi ndugu yake aliye Muislamu. Maisha yake, heshima yake na mali yake vitalindwa na sheria sawa kabisa na vile vile vya Muislamu mwingine.

Lakini, huko Akhera mtu huyu atachukuliwa kuwa ni *kafir*, au kuwa yu mbaya zaidi kuliko *kafir*. Qur'ani tukufu inasema:- *Hakika wanafiki wamo kwenye tabaka la chini zaidi la Moto (wa Jahannamu). . .* (4:145)

Mu'min (مؤمن = Muumini): Istilahi hii ina matumizi mbali mbali.

Mara nyingi Qur'ani tukufu inazungumza na Waislamu ikitumia kifungu cha maneno: *Enyi mlioamini!* Bila shaka kwa kifungu hiki, neno hili litakuwa na maana ya wale wote wanaoitamka *kalimah*.

Mahali pengine, hiki Kitabu Kitakatifu kinatofautisha baina ya *Islam* na *Iman*. Kikitumia neno *Islam* kwa kuukiri tu Uislamu kimaneno, na neno *Iman* kwa itikadi iliyo shamiri bara bara.

Katika *Ahadith* (maneno na vitendo vya Mtume (s.a.w.w.) na Maimamu (a.s.)) za Kishia na maandishi ya wanavyuoni wa Kishia, neno *Mu'min* linatumika kwa *Shi'a Ithna 'ashari* anayetekeleza bara bara maamrisho ya Dini kwa vitendo.

SURA YA 5

ZARURIYAT-E-DEEN

Kila jambo likubaliwalo na wengi wa wanavyuoni wa Kisunni na Kishi'a kuwa ni sehemu ya Uislamu linaitwa *Zaruri-e-deen* (wingi wa neno hili ni *Zaruriyat-e-deen*). Hakuna tofauti yoyote kama jambo hilo linathibitishwa na Qur'ani, Hadith, *ijma'* (إجماع = Makubaliano ya pamoja juu ya jambo la kidini) au thibitisho za kiakili. Vile vile hakuna tofauti kama jambo hilo litahusu *Usul-e-deen* au *Furu-e-deen* au Maadili katika Uislamu au Utu wema.

Zururiy-e-madh-hab (Wingi = *Zaruriyat-e-madh-hab*): Kila jambo lenye kukubalika na wengi wa Ulamaa wa *madhehebu* kuwa ni sehemu ya Madhehebu hiyo linaitwa *Zururiy-e-madh-hab*. Kwa mfano: Uadilifu wa Allah, na Utakatifu wa Maimamu kumi na wawili ni miongoni mwa *Zaruriyat-e-madh-hab* za madhehebu ya *Shi'a Ithna 'ashari*.

Yeyote yule anayekataa, anayekana au kutia shaka juu ya *Zaruriyat-e-deen* yoyote huwa *kafir* na huwa najis japo anadai kuwa ni Muislamu. Hali kadhalika, yeyote yule anayekana, anayekataa au kuwa na shaka juu ya *Zaruriyat-e-madh-had-e-Shi'a* yoyote huwa Sunni japo anadai kuwa ni *Shi'a* au awe anaziamini *Usul-e-deen* tano. Kama mtu huyo akifa kabla ya kutubia, basi mbele ya Allah, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Mashia wa Ahlul-Bayt (a.s.), yule mtu wa kwanza huwa *kafir* na ni najisi na yule wa pili huwa ni Sunni. Yule wa kwanza huwa *Murtadd* (aliyeritadi) kutoka kwenye Uislamu; na yule wa pili ni *Murtadd* kutoka *madhehebu* ya *Shi'a*.

Kama tulivyoeleza katika sura iliyotangulia, yeyote yule mwenye kuikana *Zaruriyat-e-deen* au *Zaruriyat-e-madh-hab* huwa *Murtadd* iwapo tu kama atajua kwamba jambo hilo analolikana ni *Zaruriyat-e-deen* au *Zaruriyat-e-madh-hab*, au akiwa ni mtu asiyeweza kuwa msahaulifu wa jambo hili;

kwa mfano, kama mtu huyu ni mwenye elimu ya dini au amekuwa akiishi mahali ambapo majadiliano ya kidini hufanyika kila mara.

Kama mtu haikani wazi wazi *Zaruriyat-e-deen* au *Zaruriyat-e-madh-hab*, lakini tabia yake yaonesha kuwa haiamini (japo kuwa haudhihirishi huo ukafiri wake kwa sababu ya kuogopa), basi atahesabiwa kuwa yu Murtadd. Kwa mfano kama akitamka maneno ya matusi juu ya Imamu na vivyo akasema kuwa namwamini, au akaitukana Qur'ani na kisha akasema kuwa ni wajibu kuiheshimu Qur'ani.

Tutazitaja hapa baadhi ya *Zaruriyat-e-deen* ambazo hukubaliwa na Madhehebu zote mbili Shi'a na Sunni kuwa ni sehemu kuu za Uislamu. *Zaruriyat-e-deen* hizo ni hizi:

Mungu: Kuna Mungu mmoja tu (ambaye ni Allah), Aliye hai, Mwenye nguvu zote na wa tangu na tangu na wa milele. Yu Mjuzi wa yote, Mwenye kuona yote. Anatenda kila Akipendacho kwa mapenzi Yake mwenyewe. Anazungumza na Yu mkweli (katika yale ayasemayo). Hamwingii yeyote yule, Hahitaji kitu chochote, wala Hatendi uovu. Yeye ndiye aliyeuumba ulimwengu na Yeye ndiye anayeuruzuku.

Mitume: Ni *wajibu* kuuamini Utume wa Mitume waliotangulia pamoja na Utume wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.). Mitume walikuwa huru kutokana na *kufr* na (kwa tofauti fulani fulani za kiamoni zilizoelezwa kwa kirefu) walikuwa wasio na dhambi. Vile vile walikuwa huru kutokana na upungufu kama vile wa mwili au wa tabia ambao ungewafanya watu kujitenga nao.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipaa mbinguni wakati wa *Mi'raj*. Qur'ani ni neno la Allah; *Hadithi* ni asili sahihi ya *shari'ah*. Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ni Nabii wa mwisho; hakuna Nabii atakayekuja baada yake.

Ni *wajibu* kuamini kuwa kutakuwapo kuulizwa maswali kaburini, kupitia

kwa Malaika wawili, Munkar na Nakir; kutakuwepo kukamuliwa na kaburi na vile vile ni wajibu kuamini kuwa wako Malaika, Shetani na Majini.

Siku ya Hukumu: Siku moja ulimwengu utafikia mwisho. Hapo watu wote watafufuliwa ili wahukumiwe. Kuwepo siku ya Hukumu ni ukweli. Kuhamishwa kwa roho kutoka mwili mmoja kwenda mwingine ni wazo lisilo sahihi. Kila mtu atapata malipo ya amali zake njema au mbaya. Kuwepo kwa *Mizan* (Mizani), *Hisab* (hesabu ya amali), na *Sirat* (Njia, Daraja iliyo juu ya Moto wa Jahannamu) ni ukweli. Watu watapewa hati za amali kwa mikono yao ya kulia au kushoto. *Shafa'at* (Shufaa au maombezi) ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) ni ukweli. Kutubia ni *wajibu*. Pepo na moto vipo hata hivi hapa.

Furu'-e-deen: Salaat, Saum, *Hajj*, *Zakka*, *Jihad*, *Amr bil Maaruf* (kuamrisha mema) na *Nahy Anil Munkar* (kukataza maovu) pamoja na maelezo yake yaliyo maarufu kama vile rukuu ya Salaat, Sajdah ya Salaat, idadi ya rakaa n.k.) ni wajibu.

Maadili: Wema na ukweli, subira, kutosheka, kuwatendea wema wazazi, kuwatendea wema ndugu na jirani, ubaya wa uwongo, kusengenya, ubahili na kuwaasi wazazi, ukiachilia mbali matendo mengine mengi yaliyo mema na yaliyo maovu yenye kufahamika sana kwenye jamii ya Kiislamu.

Zaruriyat-e-madh-had-e-Shi'a Ithna 'ashari: Baadhi ya *Zaruriyat* za *Shi'a Ithna 'ashari* ni hizi zifuatazo:

Allah: Allah Hamlazimishi mtu kutenda amali njema au mbaya.

Maimamu: Maimamu huteuliwa na Allah. Wako Maimamu kumi na wawili tu walioongoza baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na wao ndio warithi wake wa kweli; wa kwanza wao ni Hadhrat Ali bin Abi Talib (a.s.) na wa mwisho wao ni Imamu al-Mahdi (a.s.). Hao Maimamu kumi na wawili pamoja na Bibi Fatimah (a.s.) ni watakatifu kutokana na kila dhambi na makosa kama Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) tangu mwanzoni mwa uhai wao hadi mwisho.

Imamu wa kumi na mbili, al-Mahdi, Muhammad (a.s.) mwana wa Imamu wa Kumi na moja al-Hassan al-Askari (a.s.), yu hai na hivi sasa kafichika; atadhihiri atakaporuhusiwa na Allah, kabla ya siku ya Hukumu, na ataidumisha Dola ya Allah hapa duniani, ataijaza dunia Uadilifu na usawa kama itakavyokuwa imejawa na dhuluma na uonevu.

Furu'-e-deen: Maneno *Hayya ʿa1a Khayril ʿamal* (حَیَّ عَلٰی خَیۡرِ الۡعَمَلِ) ni sehemu ya Adhana na Iqama na meneno '*as-salatu khayrum minan nawm* (اَلصَّلٰوۃُ خَیۡرٌ مِّنَ النَّوۡم) hayaruhusiwi kutiwa kwenye Adhana na Iqama. Ndoa ya *mut'a* ni halali; mke hana fungu katika ardhi, na kuhusu mali nyingine isiyosogezeka - kama vile majengo, au miti ya bustani iliyosimama, anapata moja ya nane (au robo) ya thamani yake ya mauzo lakini sio hivyo vitu vyenyewe.

JAMBO MUHIMU: Vile vile maelezo yaliyotolewa kwenye Sura ya 3 (*Usul-e-deen*) na Sura ya 4 (Madhambi Makubwa) ni miongoni mwa *Zaruriyat-e-deen* au *Zaruriyat-e-madh-had*. Hapa tumeorodhesha chache tu ili kutoa mfano. Ziko *Zaruriyat* nyingi nyinginezo katika *Furu'-e-deen* na Maadili ambazo msomaji anaombwa kuvisoma vitabu vya rejea.

Angali: Maelezo haya yamenukuliwa kutoka kitabu kiitwacho "*Tosha-e-Akherat*" cha Marehemu Syed Rahat Husayn Golpalpuri (Aliyekuwa mwalimu mkuu wa Madrasatul-Waezeen, Lucknow, India), kilichochapishwa na Mujtabai Press, Patna, India hakina tarehe ya kuchapishwa, ukurasa wa 23-29.

SURA YA 6

AINA KUMI NA NNE ZA WATU

Shaykh Ja'far Shushtari amewagawa watu katika aina kumi na nne, kutegemeana na ujuzi wao na imani (au ukosefu wao wa elimu na imani) ya *usul-e-deen*.

Aina ya kwanza: Ni mtu ambaye kabla ya kufikia utu uzima anazijua *usul-e-deen* tano pamoja na thibitisho zao za kiakili na anaziamini. Bila ya shaka yoyote ile, mtu huyu ni Muislamu na Muumini kwa haki yake mara tu afikiapo *baligh* (balehe). (Hakuna tofauti yoyote kama mtu huyo anaweza kuzielezea thibitisho hizo kwa maneno yake mwenyewe au la).

Aina ya Pili: Ni mtu ambaye, kabla ya kufikia utu uzima anaziamini kwa uaminifu zile *usul-e-deen* kwa sababu kafundishwa na wazazi wake au na mtu mwingine mwenye kuaminika na kisha akaendelea kwenye itikadi hiyo baada ya kuwa *baligh*. Kwa mujibu wa sababu zenye nguvu za kitheolojia, si vibaya kufanya hivyo. Kama mtu huyo akiendelea kwenye itikadi hiyo, bila ya kutia shaka yoyote juu ya ukweli wao, atahesabiwa kuwa ni Muumini hapa duniani na kesho huko Akhera, Insha Allah.

Aina ya Tatu: Ni mtu ajifunzae elimu ya kweli juu ya *usul-e-deen* na akaziamini bara bara. Vivyo hivyo baadaye fikara mbaya au minong'ono ya kishetani ikamjia akilini mwake ambayo hakuipenda hata kidogo - kwa kweli akahisi kusukumizwa kwenye fikara au maoni hayo. Hakuna upungufu katika dini na imani ya mtu huyo; ukweli uliopo kwamba anaumia kutokana na fikara hizo wenyewe ni uthibitisho kwamba imani yake ina nguvu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Maimamu (a.s.) wametueleza dawa ya maradhi haya. Kila mtu huyu anaposumbuliwa na fikara hizo aseme:
(Hakuna Mungu ila Allah; tunamwamini Allah na Rasuli wake; na hakuna uwezo wala nguvu ila kwa Allah tu).

Aina ya Nne: Ni mtu ambaye alipofikia utu uzima, alianza kuzichunguza *usul-e-deen* na baada ya siku chache akapata uhakika juu ya ukweli wake, iwe kwa thibitisho za kiakili au kwa sababu ya mtu fulani mwenye kuaminika amemshawishi mpaka akavuka. Hapana shaka kwamba, baada ya kujipatia uhakika, mtu huyo atakuwa Mu'mini. Tatizo likubalikalo ni kuhusiana na muda ambao mtu huyu alikuwa akijishughulisha kujitafutia uhakika huo. Kama akifa kwenye kipindi hiki, hataadhibiwa huko Akhera. Na kama, kabla ya kufikia utu uzima alikuwa akihesabiwa kuwa ni Muislamu - kutokana na "taba'iyat" - watu wataendelea kumhesabu kuwa ni Muislamu. Lakini itakuwa vigumu kuamua kama alikuwa Muislamu hasa katika kipindi hicho.

Aina ya Tano: Ni mtu ambaye hakujipatia itikadi kamili juu ya *usul-e-deen* kabla ya kufikia utu uzima - kwa njia ya mafundisho ya wazazi au watu wengine – na ni mwenye fikara potevu (msahaulifu) juu ya dini na itikadi zake. Mtu huyu hatahesabiwa kuwa ni Muislamu, na vile vile ni vigumu kumhesabu mtu huyu kuwa ni *Tahir* (Tohara).

Ni jukumu la wazazi au mlezi kumfundisha mtoto wake mambo muhimu ya dini yake na kisha kumwongoza aisome *Kalimah* ili kwamba aweze kuwa Muislamu na *Tahir*.

Aina ya Sita: Ni mtu azijuaye na aziaminiye *usul-e-deen* zote, lakini hawezi kuzieleza kwa maneno yake mwenyewe - kama walivyo watu wengi waishio kwenye sehemu za mashambani ya mbali ambao hawawezi kuelezea ni kwa nini Allah ni mmoja tu; Au watu wengi waishio katika sehemu za mjini wasioweza kuzipata sifa zimpasazo na sifa zisizompasa Allah - lakini kama ukiwauliza kama Allah ni Mwenye Nguvu zote, watakujibu "Ndio" au kama Allah anaweza kuonekana watakujibu "Hapana". Watu hawa ni *mu'min*, na kiwango hiki cha elimu na itikadi kinatosha.

Aina ya Saba: Ni mtu tumjuaye kuwa anaisoma *Kalimah* na anasema kuwa anauamini Upweke wa Allah na Utume wa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w.). Lakini hatuna uhakika kuwa kweli anaamini

hivyo. Tunamhesabu mtu huyo kuwa ni Muislamu; hatuwajibiki kuchunguza ndani ya moyo wake, na tunaweza kusema juu yake: Ewe Allah! Hatujui chochote juu ya mtu huyu ila yaliyo mema tu, yaani tuajua kuwa ni Muislamu.

Lakini ni lipi lile lililo wajibu juu yake mwenyewe? Ni lazima athibitishe kama itikadi yake ni ya kiaminifu. Kama siyo hivyo, basi atahitajika kuisahihisha itikadi yake na kujipatia itikadi iliyo sahihi.

Aina ya Nane: Ni mtu mwenye kuisoma *Kalimah*, lakini baadaye akatambua kuwa ana shaka juu ya *tawhid* au *nubuwwat* ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) au *Qiyamat*. Kama akiwadhihirishia watu shaka yake hiyo, atahesabiwa kuwa ni *Kafir* na Najis.

Kama mtu huyo haidhihirishi shaka yake hiyo kwa maneno, lakini matendo yake na tabia zake vinaonyesha kuwa ana shaka juu ya kuwepo Upweke wa Allah au Utume wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) au siku ya Kiyama – basi, kufuatana na thibitisho zenye nguvu – ni haramu kwa mwanamke wa Kiislamu kuolewa na mtu huyu. Na ni *ahwat* kumhesabu kuwa ni *Najis* na kutokula mnyama aliyechinjwa na mtu huyu.

Aina ya Tisa: Ni mtu asiye na itikadi iliyo madhubuti juu ya kuwepo Upweke wa Allah au juu ya Utume wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) au *qiyamat* - bali anao mwelekeo wa nguvu tu juu ya vitu hivi. Swali linaloibuka ni kuhusiana na wajibu wake yeye mwenyewe juu ya jambo hili na Waislamu wengine wamtendee nini mtu huyu.

Ama kuhusu yeye mwenyewe: Kama anaweza kujipatia itikadi thabiti juu ya mambo tuliyoyataja hapo juu, na vivyo anaacha kufanya hivyo, basi hukumu ni kama ile ya mwenye kutia shaka (Namba saba hapo juu), na Kesho huko Akhera hatapata Wokozi.

Lakini kama hawezi kujipatia uhakika zaidi juu ya mambo haya hata baada ya kujitahidi sana, basi hawezi kuadhibiwa katika siku ya Hukumu, lakini hatahesabiwa kuwa ni Muislamu hapa duniani.

Na ni *ahwat* kutomwozesha mwanamke wa Kiislamu, au kula mnyama aliyechinjwa na mtu huyu, na ahesabiwe kuwa ni Najis.

Aina ya Kumi: Ni mtoto wa Muislamu ambaye kabla ya kufikia utu uzima na kabla ya kujipatia itikadi sahihi akapatwa na wenda wazimu (ukichaa); huyu ataendelea kuhesabiwa kuwa yu Muislamu. Hukumu hii hii ndiyo itakayofuatwa kuhusiana na mtoto wa mtu asiye Muislamu, ajipataye itikadi sahihi, japo kabla ya kufikia Utu uzima kisha akapatwa na wenda wazimu; vile vile ndiyo itakayofuatwa kuhusiana na mtu aliye *baligh* mwenye itikadi ya kweli kisha akapatwa na wenda wazimu. Watu wa aina zote hizi tatu watahesabiwa kuwa ni Waislamu.

Kama mtoto wa Muislamu akafikia utu uzima, kisha akawa mwenda wazimu, kabla ya kujipatia itikadi sahihi, basi hatahesabiwa kuwa ni Muislamu au *Tahir* (isipokuwa pale atangazapo kuwa ni Muislamu na kisha akawaficha watu ukosefu wake wa itikadi). Hukumu hii hii ndiyo itakayofuatwa kuhusiana na mtoto ambaye baada ya kufikia *baligh* ataanza kujitafutia itikadi sahihi lakini akapatwa na wenda wazimu kabla ya kujipatia itikadi sahihi.

Aina ya Kumi na Moja: Ni *Mustad'afin* miongoni mwa watu wasio Waislamu na wasio Shi'a.

Maana ya kawaida ya neno *Mustad'afin* ni wanyonge. Katika istilahi za kitheolojia neno hili lina maana ya wale watu ambao itikadi yao haina nguvu – yaani wale watu ambao itikadi yao haikusimama kwenye msingi wa elimu na uthibitisho.

Watu hawa wana aina mbili:
(a) Wale wapotovu wa fikara na
(b) Wale wajinga.

(a) Wapotovu wa fikara: (Wasahaulifu wa wajibu wao juu ya diin). Hawa ni wale watu ambao katu hawajawahi kufikiria kuwa wanapasika kujitafutia au

kuzisahihisha itikadi zao, wala katu hajapatikana mtu wa kuwakumbusha juu ya jambo hili.

(b) Wajinga: (Mwenye kuzubaa): Hawa ni wale watu wasio wenda wazimu wala wenye elimu, wala haiwezekani kwao kujipatia itikadi ya Kielimu.

Mustad'afin wa watu wasio Waislamu, kama vile waeskimo wa kanada na Mbilikimo wa Zaire. Hukumu juu ya watu hawa ni kama ifuatavyo hapa chini: Hawa watahesabiwa kuwa ni *Kafir* hapa duniani; lakini ni kinyume na Uadilifu wa Allah kuwaadhibu huko Akhera. Ni kweli kwamba hawawezi kuiingia Pepo. Hawa ni lazima wawekwe *A'raf* (paka uliopo baina ya Pepo na Moto), au watapewa mtihani katika siku ya hukumu na kisha watiwe Peponi au Motoni kutegemea na matokeo ya mtihani huo.

Mustad'afin wa watu wasio-Shi'a. Huko Akhera hali yao itakuwa kama ile ya *Mustad'afin* wa watu wasio Waislamu. Lakini, hapa duniani watahesabiwa kuwa ni Waislamu kwa ujumla.

Aina ya Kumi na Mbili: Ni *Mustad'afin* wa Kishia: Katika aina hii huingizwa wale wote wenye kuiamini *tawhid* na *nubuwwat*, na wenye kukubali kuwa Hadhrat Ali (a.s.) alikuwa Imamu wa kwanza, lakini hawayajui majina na mfuatano wa Maimamu (a.s.) au hawajui Imamat ni nini - ili mradi tu ni wapotevu wa fikara (ni wasahaulifu wa wajibu wao juu ya dini) au wajinga, na hawakudhamiria kuacha kujitafutia elimu hii.

Bila shaka watu hawa ni *tahir* kwa sababu wanaiamini *tawhid, nubuwwat* na *qiyamat*; Vile vile hawataadhibiwa huko Akhera - inawezekana kwamba wapelekwe Peponi pia. Lakini suala liibukalo ni kama wao wanaruhusiwa kuzipata haki zote za Waumini hapa duniani au la. Kwa mfano ni *ahwat* kutowapa kitu chochote kutokana na *kaffarah* na *radd-e-mazalim*. Vile vile wasipewe *zakat* kutokana na mafungu ya maskini au *miskin* - ingawa wanaweza kupewa kutokana na fungu la "Njia ya Allah" kama faida ya kidini inaweza kupatikana kutokana na kufanya hivyo. Inawezekana kuwapa kutokana na *fitrah* pia.

Aina ya Kumi na Tatu: Aina tuliyoitaja hapo juu inazungumzia juu ya wale *Mustad'afin* wa Kishi'a waliokuwa wapotovu wa fikara au wajinga. Sasa tunamjia mtu aliyeuingia Ushi'a, ambaye si mpotovu wa fikara wala mjinga lakini vivyo anadharau kujipatia elimu ya muhimu juu ya Maimamu kumi na wawili, hawajui majina yao, mfuatano wao au habari zao za muhimu.

Kama tulivyoeleza katika aina ya kumi na mbili, mtu wa aina hii ni *tahir* kwa sababu anamwamini Allah, Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) Siku ya hukumu, lakini ni vigumu kusema kwamba mtu huyu ataokolewa huko Akhera – - - hasa pale aikosapo elimu juu ya Imamu wa Zama zetu hizi, au hauamini uhai wake na *ghaybat* (kughibu) yake au hauamini ukweli uliopo kwamba ni Hujjat (Hoja au uthibitisho) wa Allah kwa viumbe wake. Hali kadhalika iwapo kwa uzembe wake ataacha kujitafutia elimu na itikadi hii.

Aina ya Kumi na Nne: Wenye kuritadi: Hawa ni watu walioikubali dini ya kweli, na kisha wakaikana. Hawa wanaitwa *Murtadd*, na hali yao ni mbaya kuliko zote, hukumu juu yao ni ngumu zaidi kuliko za *Kuffar* wa kawaida. Maelezo juu ya *Murtadd* yameelezwa kwenye Sura ya 4 hapo juu. Mambo fulani fulani yaliyo muhimu yanaongezewa hapa chini.

(A) Masharti ya Kuritadi: Masharti matano yafuatayo ni lazima yatimie kabla ya kumtangaza mtu kuwa ni *Murtadd*:

1. Ni lazima awe baligh (balehe)
2. Awe na akili timamu (asiwe mwenda wazimu)
3. Ni lazima akijue kile anachokizungumza. Kama neno la *Kufr* (kufuru) likimtoka ulimini mwake, pasi na kukusudia kufanya hivyo, halitachukuliwa dhidi yake.
4. Ni lazima ajue kwamba neno alilolitamka ni neno la *Kufr* na kisha alitumie kwa maana hiyo. Kama akizungumzia neno la *Kufr* bila ya kulijua maana yake au akalitumia kwa maana nyingine iliyo halali, basi halichukuliwi dhidi yake. Kama alijua kuwa ni neno la *Kufr* kisha akalitumia kwa maana hiyo, atakuwa *Murtadd* na *Najis* japo asiyajue matokeo ya matamshi yake hayo.

5. Alitamke neno la *Kufr* kwa kupenda kwake mwenyewe. Kama alilazimishwa kuyatamka maneno hayo, na akafanya hivyo ili kuyaokoa maisha yake (yaani alifanya hivyo kwa *Taqiyyah*), basi maneno hayachukuliwi dhidi yake.

(B) Kuritadi Kunaweza kwa njiaya moyo, ulimi na/au kiendo:

Kuritadi kwa Moyo: Huku humtokea kama mtu akiritadi baada ya kuamini, au akitaia shaka baada ya kuwa na uhakika.

Kuritadi kwa Ulimi: Huku humtokea wakati mtu anapokana kuwepo kwa Allah au Upweke Wake, au anapo ukana Uadilifu wa Allah au Elimu Yake n.k.; au akajaribu kuonyesha kwamba Allah hutenda matendo Yake pasi na shabah maalumu au kinyume na busara au akaikataa yoyote miongoni mwa zile *Zaruriyat-e-deen* kama vile Sala, Funga, Zakka, Hajj au akaikashifu dini, Qiyamat, Qur'ani au hadithi.

Maelezo: Baadhi ya watu husema wanapoomba Dua: "Imamu Husayn (a.s.) na akujaalie maisha marefu", au "Hadhrat Abbas (a.s.) na akuzidishie riziki yako" au "Imamu Ali (a.s.) na akujaalie watoto" au "Shahidi fulani akuhifadhi kutokana na shida." Hapa huibuka swali, kama kusema hivyo ni sawa au la.

Jibu: Kama nia hawa ni watu hawa ni kusema kuwa "Nauzipate faida hizo kwa *barakat* au *wasilah* wa watu hao watakatifu," au "Watu hao na wakuombee kwa Allah ili kwamba Yeye Allah akupe watoto, akuzidishie riziki yako au akujaalie maisha marefu" basi ni vizuri sana. Lakini kama maana yao, ni kwamba watu hao, Allah na atusamehe, ni wenye kuruzuku au waumbaji, basi jambo hili litakuwa gumu sana.

Kuritadi kwa kitendo: Natuseme mtu fulani ana itupa chini Qur'ani (kwa nia ya kuitukanisha), au kwa nia hiyo anaiopasua-pasua au anaipiga teke au anaitupilia kwenye sehemu chafu, hukumu hii hii ndiyo itakayotumika kama mtu akikitukanisha kitabu cha Dua au cha Hadithhi, au cha Majina ya Allah.

(C) Mambo matatu yamkafirishayo mtu: Yako mambo matatu ambayo, bila ya kuwepo tofauti yoyote ni kimaoni (baina ya wanavyuoni wa kidini), humfanya mtu kuwa *kafir*. Mambo hayo ni haya:

i. Kuikana yoyote miongoni mwa *Zaruriyat-e-Deen*. Mifano yake imeonyeshwa kwenye Sura ya 5 hapo juu.
ii. Kuikataa amri yoyote ya Allah. Ni kwa sababu ya kosa hili kwamba Shaytan amekuwa *kafir*, vinginevyo, yeye alikuwa akimwamini Allah, Qiyamat na karibuni amri zote za Allah; lakini yeye alipinga amri moja ya Allah na akawa *kafir* na Mlaaniwa. Alilolikataa ni kuwa: Kwa nini umeniamrisha kumfanyia Sajdah Adamu, ambapo mimi ni bora kuliko yeye.

Kuidharau amri yoyote ya Allah japo iwe ni sheria ya Sunnah. Kwa mfano ni Sunnah kwamba sharubu zipunguzwe, sasa kama mtu kwa dharura akasema: "Jambo hili si lenye kuingia akilini kiasi gani?" Au "Jambo hili linahusiana vipi na *shari'ah*?" Mtu huyo atakuwa *kafir*.

Maelezo: Shaykh Ja'far Shushtari hakuwataja *Munafiqin* katika orodha hii. Lakini kwa maoni yangu, ni haki *Munafiqin* nao wangetiwa na kufanywa aina ya Kumi na Tano. Maelezo juu ya *Munafiqin* yametolewa kwenye Sura ya 4 hapo juu.

*** MWISHO***

ISBN: 9976 956 57 6

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P 20033
Dar es Salaam